JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI**

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI**

**30/01/2024**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Chemba kwa niaba ya vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO's) anawatangazia nafasi za kazi kumi na mbili (12) kama ifuatavyo.

### MSIMAMIZI WA CHOMBO CHA WATOA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII (SUPERVISOR) - NAFASI 7

**Sifa za Muombaji**

i. Awe Mtanzania mwenye akili timamu anayejua kusoma na kuandika .
ii. **Elimu**; Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne au Zaidi
iii. **Ujuzi**; Awe na elimu ya VETA Level II-III, Astashahada au Zaidi ya ufundi wa maji katika chuo kinachotambulika na serikali
iv. **Umri**; Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi miaka 40
v. Awe na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kusimamia mafundi wasaidizi
vi. Baada ya kuajiriwa awe tayari kuapa kiapo cha uadilifu katika uongozi.
vii. **Uaminifu**; Awe ni mtu mwadilifu na mwaninifu na ambaye hajapata kuhukumiwa kwa makosa ya jinai.
viii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pasipo kusimamiwa pamoja na uwezo wa kusimamia waajiriwa wengine wote wa Chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO)
ix. Awe Mtanzania anayetoka sehemu yeyote.

### MAJUKUMU YA MSIMAMIZI WA JUMUIYA

i. Atafanya kazi chini ya usimamizi wa Chombo cha watoa huduma ya Maji (CBWSO).
ii. Atakuwa ndiye Mtendaji/Msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chombo cha watoa huduma ya Maji ngazi ya jamii (CBWSO) na pia atakuwa ndiye Katibu wa Kamati ya Maji (Bodi)
iii. Kusimamia utoaji wa huduma ya Maji yenye ubora kwa wateja/wananchi.
iv. Kuandaa taarifa za uendeshaji mradi za Wiki, Mwezi, Robo Mwaka, Nusu Mwaka na Mwaka mzima na kuziwasilisha kwa kamati (Bodi) ya Maji ya chombo cha watoa huduma.
v. Kupanga na kusimamia bajeti ya uendeshaji na matengenezo ya mradi na



MENEJA WA RUWASA
CHEMBA

CamScanner

kutoa ushauri wa kiufundi kwa kamati (Bodi) ya Maji na Meneja wa RUWASA Wilaya.

vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya mradi ikiwa pamoja na mapato na matumizi.

vii. Kuhamasisha uchangiaji wa huduma ya Maji, kutatua na kusuluhisha migogoro baina ya mteja / wananchi na Chombo cha watoa huduma (CBWSO).

viii. Kufanya manunuzi ya mahitaji ya mradi kwa kufuata taratibu za manunuzi ya Umma.

ix. Kuweka na kutunza kumbukumbu zote zinazohusu uendeshaji na matengenezo.

## MHASIBU WA MRADI - NAFASI 5

### Sifa za muombaji

i. Awe Mtanzania mwenye akili timamu anayejua kusoma na kuandika

ii. **Elimu**; Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne au Zaidi

iii. **Ujuzi**; Awe na Cheti cha Astashahada ya uhasibu au zaidi

iv. **Umri**; Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi miaka 40

v. Baada ya kuajiriwa awe tayari kuapa kiapo cha uadilifu katika kazi.

vi. **Uaminifu**; Awe ni mtu mwadilifu na mwaninifu na ambaye hajapata kuhukumiwa kwa makosa ya jinai.

vii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pasipo kusimamiwa.

viii. Awe Mtanzania anayetoka sehemu yeyote

## MAJUKUMU YA MHASIBU

i. Atakuwa ndiye msimamizi wa masuala ya kifedha katika chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO).

ii. Kusimamia ukusanyaji wa malipo ya Ankara za maji.

iii. Kuandaa bajeti ya mwaka ya CBWSO.

iv. Kuandaa taarifa zote za fedha na kuziwasilisha kwa msimamizi wa CBWSO.

v. Kufanya malipo baada na kuidhinishwa na msimamizi wa CBWSO na Meneja wa RUWASA Wilaya.

vi. Kutunza vitabu vya fedha,hati za malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa mapato, malipo na matumizi ya fedha ya shughuli husika.

vii. Kupeleka fedha zote benki za makusanyo ya Ankara ya maji kabla ya matumizi.

viii. Kushauriana na msimamizi wa CBWSO (**Supervisor**) katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shughuli zote za miradi.



MENEJA WA RUWASA CHEMBA

## MASHARTI YA KAZI /MSHAHARA

i. Kazi ni ya Mkataba wa miaka 3, Mkataba unaweza kuhuishwa na **Mwajiri Ambae ni Chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO)** kutokana na utendaji kazi mzuri wa Mhusika.
ii. Malipo ya Mshahara kwa Mwajiriwa **yatatokana na Makusanyo/mauzo ya Maji ya Chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO) husika.**
iii. Muombaji awe tayari kufanya kazi katika Chombo cha watoa huduma ya maji chochote atakachopangiwa katika Wilaya ya Chemba.

## MAELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

Muombaji aandike barua ya maombi kwa mkono (Waombaji wanawake wanahamasishwa kuomba na watapewa kipaumbele) barua ya maombi iwe na viambatanisho vifuatavyo;

i. Wasifu wake - Curriculum vitae
ii. Nakala za vyeti mbalimbali vya kitaaluma (kidato cha nne, ujuzi n.k)
iii. Picha ndogo (*Passport size*) mbili (2) zilizopigwa hivi karibuni.
iv. Kivuli cha kitambulisho cha Uraia (NIDA) au Kadi ya Mpiga kura.
v. Majina, anuani na mawasiliano ya wadhamini (*referees*) wawili (2).

Aidha maombi ya kazi yanaweza kutumwa kwa kutumia **barua pepe; chembadm@ruwasa.go.tz. Au** barua za maombi ziwasilishwe kwa mkono kwa kuletwa moja kwa moja Ofisi ya Meneja wa RUWASA Wilaya ya Chemba (zilizopo ndani ya yard ya CHICO mkabala na ofisi ya TARURA Wilaya) ama zitumwe kwa njia ya Posta kwa Anuani ifuatayo:-

**MENEJA RUWASA (W),**
**S.L.P 36,**
**CHEMBA.**

## MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI:

Mwisho wa kupokea barua za maombi itakuwa ni **siku ya Jumatano tarehe 14 February, 2024 saa 9:30 Alasiri.**

Maombi yote yatakayowasilishwa baada ya muda huo hayatapokelewa.

Tangazo limetolewa na;

MENEJA WA RUWASA
CHEMBA

**MENEJA WA RUWASA,**
**WILAYA YA CHEMBA.**



CS CamScanner